

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA**



MKOA: LINDI

SIMU: 0782336592
0658733999

SHULE YA SEKONDARI YA MTANGA,
S.L.P. 134,
KILWA MASOKO.
14/12/2020.

KUMB: NA. MTSS/2656/VOL.1/2021

MZAZI/MLEZI WA
KUTOKA SHULE YA MSINGI
MKOA WA.....WILAYA YA

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA MTANGA ILIYOPO
HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA MKOA WA LINDI KWA MWAKA 2021**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao mtajwa hapo juu amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Shule ipo umbali wa makadirio ya kilometa 7 kutoka stendi ya mabasi ya Mji Mdogo wa Kilwa Masoko kuelekea njia iendayo Dar es Salaam.

Usafiri kutoka kituo cha mabasi katika mji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa hadi shuleni unapatikana kwa shilingi 200/- kwa mwanafunzi na shilingi 1000/- kwa watu wengineo.

Muhula wa masomo unaanza tarehe 11/01/2021. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni siku saba baada ya tarehe ya kuanza muhula wa masomo.

Napenda kuisisitiza kufanya maandalizi mapema juu ya mahitaji ya mwanao ili aweze kuripoti kwa wakati na kuwahi masomo sambamba na wenzake. Kwa kuwa ada na michango mbalimbali imefutwa kupitia mpango wa serikali ya awamu ya tano wa utoaji wa Elimumsingi bila malipo, natumaini kwamba utamwanda mwanao ili aje kuripoti kwa wakati.

Pamoja na barua hii nimeambatanisha fomu zifuatazo ili uzishughulikie haraka na kuzirejesha shuleni mapema iwezekanavyo au siku ya kuripoti.

- Fomu namba 1: Mambo muhimu ya kuzingatia
- Fomu namba 2; Fomu ya kupima afya ya mwanafunzi
- Fomu namba 3; Taarifa za mzazi/mlezi na taarifa za mwanafunzi

Aidha, kila mwanafunzi alete nakala ya cheti cha kuzaliwa siku ya kuripoti shuleni.

KARIBU SANA MTANGA SEKONDARI

**JONAS H RUAMBO
MKUU WA SHULE**

FOMU NAMBA 1: MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

1.1.0 Sare za shule (School Uniform)

Mwanafunzi anatakiwa awe na Sare iliyo sahihi na inayokubaliwa na uongozi wa shule.

a) Wavulana

- Suruali mbiliza Ton Red (Damu ya mzee) mshono wa rinda. Jeans stail haitakubalika.
- Mashati mawili meupe mikono mifupi
- Viatu vyeusi jozi mbili
- Soksi nyeupe Jozi mbili
- Mkanda mweusi wa ngozi

b) Wasichana

- Sketi mbili rangi ya Ton Red (Damu ya Mzee) Linda box
- Mashati/blauzi mbili nyeupe zenye mikono mifupi
- Viatu vyeusi jozi mbili
- Soksi ndefu nyeupe Jozi mbili
- Kwa wanafunzi waislamu wanaruhusiwa kuvaa HIJABU nyeupe ya kawaida isio na Mapambo. Hijabu hiyo iwe ya duara.

NB:

- Viatu na soksi visiwe vya rangi, Madoa, Mistari wala mapambo ya aina yoyote, pia viatu visiwe vya kupanda (ngazi) wala mabuti au yebo yebo.
- Haturuhusu kuvaa kofia, Kanda mbili, mapambo ya aina yoyote ile kama Bangili, mkufu, pete, heleni, irizi, n.k Vilevile mwanafunzi haruhusiwi kunyoa kipara bila sababu inayokubalika na utamaduni wa kiafrika au bila ruhusa maalumu.

c) SARE ZA MICHEZO

Kila mwanafunzi awe na sare ya michezo kwa ajili ya kuimarisha afya yake. Kwa shule hii, sare ya michezo ni kama ifuatavyo:-

- **WASICHANA**
Tracksuit rangi ya blue
Viatu vya michezo
- **WAVULANA**
Tracksuit rangi ya blue au bukta na T-shirt rangi ya Blue
Viatu vya michezo

1.2.0 VIFAA VYA DARASANI/TAALUMA

Mwanafunzi wa kidato cha kwanza anatakiwa kusoma kwa lazima masomo Tisa (9) ambayo ni:-

- CIVICS
- HISTORY
- GEOGRAPHY
- KISWAHILI
- ENGLISH
- PHYSICS
- BIOLOGY
- CHEMISTRY
- BASIC MATHEMATICS

Hivyo, kila mwanafunzi aje na vifaa vya kuendeleza taaluma vifuatavyo:-

- a) Madaftari tisa (9) na kalamu za kutosha pamoja na mkebe wa hesabu (Mathematical set).
- b) Rimu moja
- c) Unashauriwa kuwa na kamusi (Dictionary) yako binafsi itakayokusaidia wakati wote kupata tafsiri ya misamiati mbalimbali katika lugha.

1.3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

1.3.1 Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995 . Aidha , inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni

- a) Heshima kwa viongozi , wazazi, wafanyakazi wote , wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni.
- d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wowote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- f) Kutunza usafi wa mwili , mavazi na mazingira ya shule.
- g) Kuvaa sare za shule wakati wowote unapotakiwa .
- h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
- i) Kutunza mali za umma.

1.3.2 MAKOSA YAFUATAYO YANAWENZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

- a) Wizi
- b) Uasherati na ushoga
- c) Ubakaji
- d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
- e) Kupigana au kupiga
- f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- g) Kudharau bendera ya Taifa au wimbo wa Taifa.
- h) Kuwa mjamzito/ kupata mimba.
- i) Kuoja au kuolewa
- j) Kutoa mimba
- k) Kugoma , kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- l) Kukataa adhabu kwa makusudi
- m) Kuwa na simu ya mkononi.

1.3.3 VIFAA VYA USAFI NA UTUNZAJI WA MAZINGIRA

Kwa kuzingatia umuhimu wa usafi binafsi kwa kila mwanafunzi na usafi wa mazingira ya shule kwa ujumla, utatakiwa kuja na vitu vituatavyo:-

- a) Uje na mche mmoja wa mgomba au mkorosho au muembe kwa ajili ya kuendeleza bustani ya shule. Mwanafunzi atasimamia mti wake ili uweze kukua bila kunyauka.
- b) Jembe moja lenye mpini kwa ajili ya usafi wa mazingira ya shule kama vile kuchimba mashimo ya taka, kulimia njia za ndani ya shule na usafi wa bustani ya shule
- c) Panga moja lenye mpini na lililonolewa kwa ajili ya kupangulia miti ili iwe na mwonekano mzuri na wa kupendeza hapa shuleni.
- d) Fyekeo lenye mpini na lililonolewa kwa ajili ya usafi wa kufyeka nyasi hasa masika.
- e) Ndoo ndogo moja kwa ajili ya kuchotea maji ya kumwagia bustani, kudeki madarasani na vyooni na kutunzia maji ya akiba ya kutumia wanafunzi kwa ajili ya kunywa na kunawa.
- f) Fagio moja la wima kwa ajili ya kufagia taka katika maeneo ya shule.

NB: Wanafunzi wote wanatakiwa kuripoti kwa wakati bila kujali changamoto zao ambazo zitaendelea kushughulikiwa na wazazi/walezi wao wakati masomo yakiendelea.

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENT'S OFFICE, REGIONAL ADMINISTRATIVE AND LOCAL GOVERNMENT
KILWA DISTRICT COUNCIL**



REGION: LINDI

PHONE: 0782336592
0658733999

MTANGA SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 134,
KILWA MASOKO.
14/12/2020

KUMB: NA. MTSS/2656/VOL.1/2021
FORM NO 2:

To the medical officer

.....
.....

RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION OF MR/MISS

Please examine the above named pupil and give us the report regarding his/her suitability for undertaking secondary school education as a student on the following grounds:

1. Pupil full name Age.....
2. Blood.....
3. Stool
4. T.B. Test
5. Syphilis
6. Urine examination
7. Eye test.....
8. Chest test.....
9. Ears test.....
10. Spleen
11. Abdomen.....
12. Pregnancy test (for girls only)

ANY ADDITIONAL INFORMATION E.g. physical defects or impairment, infection, family diseases, etc.....
.....

I certify that, the above named pupil is suitable/unsuitable for secondary school studies. If unsuitable give reasons

NAME OF MEDICAL OFFICER..... DATE.....

SIGNATURE AND OFFICIAL STAMP.....

OFISI YA RAIS TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA



MKOA: LINDI

SIMU: 0782336592
0658733999

SHULE YA SEKONDARI YA MTANGA
S.L.P. 171,
KILWA MASOKO.
14/12/2020

KUMB: NA. MTSS/2656/VOL.1/2021

FOMU NAMBA 3.

A: TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI

1. Jina kamili la mzazi/mleziJinsi.....
2. Kazi afanyayo
3. Anuaninamba ya simu
4. Mkoa wilayatarafa
5. Katakijiji.....mtaa/kitongoji

Mimi mzazi/mlezi wa mwanafunzi..... ninaahidi kushirikiana na walimu pamoja na watumishi wote wa shule ya Sekondari Mtanga katika kumlea mwanangu kwa muda wote atakapokuwa shuleni na kwamba:-

- a) Ninaahidi kumpatia vifaa vyote vinavyohitajika shuleni ikiwa ni pamoja na chakula, mahali pa kulala na mahitaji mengine kwa wakati wote mpaka amalize masomo yake.
- b) Ninaahidi kushirikiana na walimu kuhakikisha kwamba, mwanangu anafuata sheria na taratibu zote za shule, na pale atakaposhindwa, hatua ipasayo ichukuliwe dhidi yake
- c) Ninaahidi kumdhibiti mwanangu asiwe mtoro shuleni
- d) Mwanangu akiwa shuleni alelewe katika dini ya
- e) Nitaomba kujulishwa mara kwa mara endapo mwanangu ameenda kinyume na taratibu za shule na nitakuwa tayari mwanangu kupewa adhabu inayostahili kwa makosa atakayofanya.

Jina la mzazi/mleziSahihi..... Tarehe

B: TAARIFA ZA MWANAFUNZI (IJAZWE NA MWANAFUNZI MWENYEWWE)

Jina la mwanafunzi:.....Jinsi.....Shule ya msingi.....

1. Je, una tatizo la kiafya linalohitaji uangalizi wa karibu? (litaje kama lipo).....
2. Unalewa mashetani (ndio/hapana)..... kama ndio tangu lini?.....
3. Vipaji/Michezo/sanaa anayopendelea

Na.	Jina la Kipaji/mchezo/Sanaa	Na	Jina la Kipaji/mchezo/Sanaa
1		3	
2		4	

4. Nafasi yoyote ya uongozi aliyowahi kushika

Na.	Aina ya uongozi	Shule	Mwaka
1			
2			
3			

5. Umewahi kupitia mafunzo ya SKAUTI shuleni kwako? Ndiyo Hapana

Nathibitisha kwamba taarifa nilizozitoa hapo juu ni za kweli, pia nathibitisha kuwa nitakuwa na tabia nzuri, mchapa kazi pamoja na kuwa na bidii ya masomo.

Ni mimi MwanafunziSahihiTarehe.....